# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 29/10/2021 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI.

**Mahudhurio ya Wajumbe**

| NA | JINA KAMILI | CHEO | WADHIFA |
|---|---|---|---|
| 01 | Mhe. Japhael M. Lufungija | Diwani Kata ya Ilege | Mwenyekiti |
| 02 | Bw. Jerry D. Mwaga | Mkurugenzi Mtendaji Wilaya | Katibu |
| 03 | Mhe. Aloyce A. Kwezi | Mbunge Jimbo la Kaliua | Mjumbe |
| 04 | Mhe. Rehema J. Migilla | Mbunge Jimbo la Ulyankulu | Mjumbe |
| 05 | Mhe. Abdallah H. Mbuguma | Diwani Kata ya Ufukutwa | Mjumbe |
| 06 | Mhe. James M. Nundo | Diwani Kata ya Makingi | Mjumbe |
| 07 | Mhe. Anastazia D. Bebete | Diwani Kata ya Ushokola | Mjumbe |
| 08 | Mhe. Emmanuel E. Lugaila | Diwani Kata ya Igwisi | Mjumbe |
| 09 | Mhe. William K. Magembe | Diwani Kata ya Kashishi | Mjumbe |
| 10 | Mhe. Jibishi. B. Kanza | Diwani Kata ya Usenye | Mjumbe |
| 11 | Mhe. Lilian E. Seleli | Diwani V/M/Ichemba | Mjumbe |
| 12 | Mhe. Zainabu S. Andrea | Diwani V/M/Zugimlole | Mjumbe |
| 13 | Mhe. Tamari D. Kavinza | Diwani V/M/Kashishi | Mjumbe |

**Mahudhurio ya wataalam**

| NA | JINA KAMILI | CHEO | WADHIFA |
|---|---|---|---|
| 01 | Bi. Flora S. Malima | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala | Mtaalamu |
| 02 | Bw. Mussa Msananga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | Mtaalamu |
| 03 | Dr. Lusubilo D. Adam | Mkuu wa Idara ya Afya | Mtaalamu |
| 06 | Bw. Lucas G. Mirambo | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | Mtaalamu |
| 07 | Bw. Theogonius E. Ligonja | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii | Mtaalamu |
| 08 | Bw. Robert R. Toyi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari | Mtaalamu |
| 09 | Bw. Jovitus C. Kamugisha | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili | Mtaalamu |
| 10 | Eng. Nyakiriga S. Warioba | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zima moto | Mtaalamu |
| 11 | Bw. Bryceson A. Kalatwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti Taka Ngumu | Mtaalamu |
| 04 | Bw. Simeon S. Twiyogohe | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | Mtaalamu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 05 | Bw. John C. Motto | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi | Mtaalamu |
| 12 | Bw.Edwin M. Mashala | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | Mtaalamu |
| 13 | Bw. Gilbert G. Rwehumbiza | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Mtaalamu |
| 14 | Bi. Dina T. Maleni | Kaimu MKuu wa Kitengo cha Sheria | Mtaalamu |
| 15 | Bw. Denis G. Nyambanila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA | Mtaalamu |
| 16 | Bi. Veronica F. Kasungi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki | Mtaalamu |
| 17 | Bw. Steward K. Eliack | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi | Mtaalamu |
| 19 | Bw. Lunyalula P. Mayenga | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi | Mtaalamu |
| 19 | Bw. Anthony J. Nsolloh | Afisa Malalamiko | Mtaalamu |
| 20 | Bw. Daniel B. Zephania | Afisa Tarafa Kashishi | Mtaalamu |
| 21 | Bw. Simon P. Malando | Afisa Tarafa Igagala | Mtaalamu |
| 22 | Bw. Mathew D. Fuko | Afisa Tarafa Kazaroho | Mtaalamu |
| 23 | Bw. Bethod S. Mahenge | Afisa Tarafa Kaliua | Mtaalamu |
| 24 | Bw. Gawaza I. Gawaza | Kaimu Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa walimu | Mtaalamu |
| 24 | Bw. Jackson K. Zacharia | Afisa Tarafa Mwongozo | Mtaalamu |
| 24 | Bw. Victor B. Msokwa | Kaimu Afisa Usafirishaji | Mtaalamu |
| 25 | Bw. Haji I. Rozzo | Mhasibu wa Mapato | Mtaalamu |

**Sekretarieti**

| | | |
|---|---|---|
| 01 | John W. Mwendo | Mwandishi wa Vikao |
| 02 | Yohana Enock Asajile | Mwandishi wa Vikao |
| 03 | Nasibu M. Iddi | Mwandishi wa Vikao |

**MUHT. NA.01/FUM/03/29/10/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao, Katibu aliwakaribisha wajumbe na wataalam kwenye kikao na baada ya kusema hayo, alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti, aliwajulisha wajumbe kuwa, kikao hicho ni cha kawaida cha robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kushauri wataalamu kujibu vizuri maswali yatakayoulizwa na wajumbe ili kuweza

kuelewa vizuri na kuwa na majawabu ya kuwasaidia wanapoulizwa na wananchi. Baada ya kusema hayo, alifungua kikao saa 08:00 mchana.

**MUHT.NA.02/ FUM/03/29/10/2021/2022: KUSOMA NA KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO**

Agenda ziliwasilishwa na Katibu kama zilivyoandaliwa, wajumbe walikubaliana agenda mbili ziondolewe na agenda mbili ziongezwe ambapo waliongeza agenda ya ombi la kuongezewa mkataba wa zabuni wa kutoa huduma ya usafi katika mji wa Kaliua, Ushokola na Ulyankulu na taarifa ya ISAWIMA. Baada ya kuongeza agenda hizo na kuwasilisha wajumbe walipokea na kuridhia agenda hizo kama ifuatavyo;

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na kuridhia agenda za kikao
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 14/09/2021
4. Kupitia Utekelezaji wa Yatokanayo na kikao kilichopita cha tarehe 14/09/2021
5. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao maalumu cha Kupokea, Kujadili na Kutoa maoni kuhusu kitabu cha Hesabu za Mwisho za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilichopita cha tarehe 25/09/2021
6. Kupokea, Kujadili na Kupitisha Taarifa ya Fedha, Mapato na Matumizi mwezi Septemba, 2021.
7. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Robo ya Kwanza kuanzia Julai 2021 hadi Septemba 2021
8. Kupokea, Kujadili na Kupitisha Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022
9. Kupokea, Kujadili na Kupitisha Mapendekezo ya Kuvuna Magogo ya Miti aina ya Mkurungu kutoka kwenye Msitu wa Hifadhi wa Ulyankulu
10. Kupokea, Kujadili na Kupitisha Mapendekezo ya mabadiliko ya bei za Viwanja Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua
11. Kupokea na Kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu
12. Kupokea Taarifa ya Mapokezi ya gari lenye namba za usajiri **SU 36793** lililokuwa mali ya **PSSSF**.
13. Maombi ya Idhini ya Kutumia fedha **Sh. 23,400,000/=** kwa ajili ya matengenezo ya gari lenye namba za usajiri **SU 36793**

14. Kupokea na Kujadili Taarifa ya makisio ya ujenzi wa kituo cha afya Igagala kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje, maabara na kichomea taka
15. Kupitia na kuidhinisha taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli za Idara na Vitengo kipindi cha April hadi Juni, 2021
    15.1. Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji
    15.2. Idara ya Utumishi na Utawala
    15.3. Idara ya Fedha na Biashara
    15.4. Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani
    15.5. Kitengo cha TEHAMA
    15.6. Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
    15.7. Kitengo cha Sheria
    15.8. Kitengo cha Uchaguzi
16. Kupokea, kujadili na Kupitisha Taarifa ya zabuni mbalimbali zilizopitishwa na Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya kaliua
17. Kupokea, Kupitia na Kujadili maoni ya Kamati ya Ukaguzi kuhusu taarifa ya Mkaguzi wa Ndani robo ya kwanza Julai – Septemba 2021 (2021/2022)
18. Taarifa za Serikali

    i. *Taarifa ya Mapokezi ya Fedha **Sh. 3,700,000,000.00** na Ombi la Idhini ya Kufanya Uhamisho wa Fedha Nje ya Bajeti (**Reallocation Between**) ya Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19*

    ii. *Taarifa ya Mapokezi ya Fedha **Sh. 368,117,139.58** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo*

    iii. *Taarifa ya Vijiji Vilivyoruhusiwa kuendelea kuwa Vijiji halali vilivyokuwa kwenye Hifadhi za Misitu ya Ulyankulu, Igombe, Mpandaline na North Ugala*

    iv. *Taarifa ya mapokezi ya Fedha sh. 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ilege*

19. Kupokea, Kujadili na Kupitisha Taarifa ya Shule ya Sekondari ya Ulyankulu kununua Vifaa vilivyopo katika Zahanati ya Makonge
20. Kupokea na Kuridhia Taarifa ya matumizi ya Vifaa vya ujenzi wa kituo cha Afya Uyowa vinavyoweza kuharibika viweze kutumika ambavyo ni mbao za kufungia "blundering"

21. Taarifa ya Ziara ya wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ya tarehe 20-24/10/2021
22. Mengineyo Kwa Idhini ya Mwenyekiti
23. Kufunga Kikao

**MUHT.NA.03/FUM/03/29/10/2021/2022/KUSOMA, KUPITIA, NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 14/09/2021**

Muhtasari uliwasilishwa na Katibu, kisha Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuupitia ukurasa kwa ukurasa. Baada ya kuupitia wajumbe walisahihisha makosa ya kiuandishi katika **MUHT. NA.01/FUM/02/14/09/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO** badala ya neno kumkaribishwa iandikwe kumkaribisha, badala ya kuandika **MUHT.NA.13/FUM/01/14/09/2021/2022 iandikwe MUHT.NA.13/FUM/02/14/09/2021/2022**. Baada ya masahihisho hayo wajumbe, walikukubaliana kuwa muhtasari usainiwe ili uwe kumbukumbu sahihi na halali ya kikao hicho.

**MUHT.NA.04/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPITIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 14/09/2021**

Yatokanayo na muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe **14/09/2021** yaliwasilishwa na Katibu kisha wajumbe walipokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na kujadili kama ifuatavyo;

**Matumizi ya salio la fedha za zidio la bakaa**

Azimio lilihusu, Fedha zilizokuwa zimependekezwa katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi shuleni, ufuatiliaji wa miradi na ununuzi wa eneo, zote kwa pamoja ziunganishwe na fedha iliyotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya ununuzi mitambo ili zitumike kununua greda la halmashauri ambapo azimio lilitekelezwa, fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi shuleni, ufuatiliaji wa miradi na ununuzi wa eneo kiasi cha **sh. 59,113,928.12** zimeelekezwa kwenye ununuzi wa greda la halmashauri

Baada ya utekelezaji huo kuwasilishwa wajumbe walipokea na kuridhia utekelezaji wa azimio.

**Ziara ya wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango**

Azimio lilikuwa, Kabla ya tarehe 25/09/2021 ifanyike ziara ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ili kukagua miradi ya ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati ambapo utekelezaji ulifanyika kwa ziara ya wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ya kukagua ujenzi wa miradi ya vituo vya afya na zahanati kufanyika kuanzia tarehe 20-24/10/2021 ambapo ziara hiyo iliunganishwa na ziara ya robo ya kwanza kwa mwaka 2021/2022.

Baada ya utekelezaji huo kuwasilishwa wajumbe walipokea na kuridhia utekelezaji wa azimio.

**Taarifa ya Orodha ya Vikundi vyote vya wajasiriamali vinavyodaiwa**

Azimio lilikuwa, Taarifa ya orodha ya vikundi vyote vinavyodaiwa iandaliwe ikionesha tarehe na mwaka waliokopeshwa, Kata na kijiji kinakotoka kikundi, kiasi walichokopeshwa, kiasi walichorejesha na fedha wanayodaiwa kisha kuiwasilisha kwenye kikao kijacho cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ambapo azimio lilitekelezwa kwa taarifa ya vikundi vyote vinavyodaiwa kuandaliwa na kuambatishwa kwenye kabrasha la kikao.

**Matumizi ya salio la fedha za zidio la bakaa kwa ajili ya tathmini ya msitu wa Ulyankulu**

Azimio lilikuwa, Fedha za zidio la bakaa zilizokuwa zimependekezwa kutumika kwenye shule ya mchepuo wa kiingereza na ujenzi wa vibanda vya stendi pamoja na fedha iliyopendekezwa kwenye tathmini ya msitu wa Ulyankulu zitumike katika shughuli ya Tathmini ya Msitu wa Ulyankulu ambapo ilielezwa kuwa, azimio limetekelezwa, Fedha za zidio la bakaa zilizokuwa zimependekezwa kutumika kwenye shule ya mchepuo wa kiingereza na ujenzi wa vibanda vya stendi pamoja na fedha iliyopendekezwa kwenye tathmini ya msitu wa Ulyankulu kiasi cha **sh. 90,000,000/=** zimeelekezwa kwenye tathmini ya msitu wa Ulyankulu. Baada ya utekelezaji huo kuwasilishwa wajumbe walipokea na kuridhia utekelezaji huo.

**MUHT.NA.05/FUM/03/29/10/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO MAALUMU CHA KUPOKEA, KUJADILI NA KUTOA MAONI KUHUSU KITABU CHA HESABU ZA MWISHO ZA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KILICHOPITA CHA TAREHE 25/09/2021**

Muhtasari uliwasilishwa na Katibu, kisha Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuupitia ukurasa kwa ukurasa na haukuwa na masahihisho. Baada ya kuupitia wajumbe waliridhia muhtasari huo usainiwe ili uwe kumbukumbu sahihi ya kikao hicho

**MUHT.NA.06/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA FEDHA, MAPATO NA MATUMIZI MWEZI SEPTEMBA, 2021.**

Taarifa iliwasilishwa na Mweka Hazina kwa niaba ya Katibu kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 imekisia kukusanya na kutumia jumla ya Tshs **37,675,212,569.47** Katika kipindi cha **Septemba 2021** Halmashauri imepokea/imekusanya jumla ya shilingi **Tshs 3,280,568,576.94** kutoka vyanzo mbalimbali.

Mapato haya ni kwa mchanganuo Ufuatao:

| | | |
|---|---|---|
| ✓ Mapato ya Ndani | **Tshs.** | **829,382,983.78** |
| ✓ Matumizi mengineyo (OC) Tshs | **Tshs** | **26,223,333.31** |
| ✓ Mishahara (PE) | **Tshs.** | **1,673,361,650.00** |
| ✓ Miradi ya maendeleo | **Tshs.** | **751,600,609.85** |

Hivyo, hadi kufikia tarehe 31/08/2021 Halmashauri ilikuwa imekusanya/imepokea mapato ya Jumla ya Tshs **8,244,170,442.44** ambazo ni sawa na asilimia **22 ya** makisio ya mwaka 2021/2022 kwa mchanganuo ufuatao:

| | | | |
|---|---|---|---|
| ✓ Vyanzo vya Halmashauri | **Tshs** | **1,746,941,247.04** | **sawa na 49%** |
| ✓ Ruzuku ya matumizi mengineyo(OC) | **Tshs** | **312,539,999.93** | **sawa na 28%** |
| ✓ Ruzuku ya mishahara(PE) | **Tshs** | **5,024,939,950.00** | **sawa na 22%** |
| ✓ Ruzuku ya miradi ya maendeleo | **Tshs** | **1,159,749,245.47** | **sawa na 11%** |

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kujadili taarifa hiyo kama ifuatavyo;

Mjumbe alipongeza kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika katika ukusanyaji wa mapato pamoja na baadhi ya kasma kufanya vizuri lakini alitaka kujua kuhusu baadhi ya kasma zilizoonekana kutokusanywa wakati katika kikao kilichopita ilielezwa kuwa zimesha fuatiliwa na zitaanza kukusanywa. Vyanzo hivyo ni kama vile mahindi, mchele na karanga. Aidha, alishauri kasma zinazoonekana kufanya vizuri ziongezewe bajeti.

Ilielezwa kuwa, makusanyo kuwa chini katika baadhi ya mazao yaani karanga na mahindi ni kutokana na wakusanya mapato kuchagua kipengele tofauti kwani kwenye baadhi ya mashine za kukusanyia mapato lilishashughulikiwa na linaendelea kushughulikiwa na katika taarifa ya fedha ya mwezi Oktoba 2021 mabadiliko yataonekana.

**Utofauti wa faini na adhabu ya leseni**

Mjumbe alitaka kujua utofauti uliopo kati ya adhabu ya leseni na faini kwani inaonekaka kufanana.

Ilielezwa kuwa, adhabu ya leseni ni fedha anayotoa mfanya biashara kutokana na kuchelewa kulipia leseni kwa muda mrefu na faini ni fedha anayolipa mtu kutokana na kufanya makosa mbalimbali kama vile kuzidisha mzigo kwenye gari.

**Ongezeko la bei za viwanja**

Mwenyekiti alitaka kujua sababu za kuendelea kuomba kufanya mabadiliko ya kuongeza bei za viwanja wakati katika taarifa ya fedha hakuna fedha iliyokusanywa kwenye uuzaji wa viwanja vya halmashauri.

Ilielezwa kuwa, fedha imekusanywa kwenye uuzaji wa viwanja na katika taarifa ya fedha ya Oktoba fedha ya uuzaji wa viwanja itaonekana.

**Usambazaji wa mashine mpya za kukusanyia mapato (POS Mashine)**

Mjumbe alitaka kujua iwapo mashine za kukusanyia mapato zilizonunuliwa hivi karibuni zimeanza kusambazwa kwa ajili ya kuanza kukusanyia mapato.

Ilielezwa kuwa, mashine za kukusanyia mapato ambazo zimenunuliwa hivi karibuni zimeanza kusambazwa na zimepelekwa kwenye mageti makubwa kutokana na ubora wa mashine hizo ambazo haziwezi kutumika kwenye udanganyifu wa kutoa risiti feki.

**Matumizi ya mzani wa Kashishi**

Mjumbe alishauri kuwa, wataalam wafuatilie mzani wa halmashauri uliopo kwenye geti la Kashishi kwani unaonekana kutumika isivyo.

Ilielezwa kuwa, litafuatiliwa ili kuweza kubaini kinachoendelea katika matumizi ya mzani uliopo katika geti la Kashishi.

Mwenyekiti alieleza kuwa suala la mzani wa Kashishi liendelee kufuatiliwa ili kuweza kubaini kinachoendelea.

**Mgao wa vifaa vya ujenzi vinavyonunuliwa na Halmashauri**

Mwenyekiti alieleza kuwa mgawanyo wa fedha kwa 40% kwa 60% uzingatiwe na baada ya kununua vifaa vya ujenzi hasa saruji maeneo yasiyopitika wakati wa masika kama vile Usinga yapewe kipaumbele ili vifaa vifike mapema kwenye maeneo hayo kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza.

**MUHT.NA.07/FUM/03/29/10/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA ROBO YA KWANZA KUANZIA JULAI 2021 HADI SEPTEMBA 2021**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai 2021 -Septemba, 2021) Hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2021 Halmashauri ilikuwa imepokea jumla ya **Tsh. 1,207,184,324.01** kati ya **Tsh. 11,616,323,239.00** zilizoidhinishwa kwa matumizi ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 sawa na asilimia **10**.

Kati ya fedha zilizopokelewa **Sh. 896,813,463.30** zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali sawa na asilimia **8** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, matumizi ya fedha yaliyofanyika ni sawa na asilimia 78 ya fedha zilizopokelewa. Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo;

**Ujenzi wa shule ya mchepuo wa kiingereza**

Mwenyekiti alieleza kuwa, mradi wa shule ya mchepuo wa kiingereza usiendelee kutekelezwa hadi Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango itakapowasilishiwa tathmini ya michoro ya ujenzi wa shule ya mchepuo wa kiingereza. Aidha, Mwenyekiti alishauri kuanza na kidogo yaani majengo ya kawaida kabla ya kuanza na majengo ya ghorofa wanafunzi watakapokuwa wameanza kusoma majengo ya ghorofa yatajengwa baada ya kupata fedha.

**Azimio**

Mradi wa ujenzi wa shule ya mchepuo wa Kiingereza umesitishwa hadi Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango itakapowasilishiwa tathmini ya michoro ya ujenzi wa shule hiyo.

**Fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali**

Mjumbe alishauri kuwa, kutokana na fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa kupewa baadhi ya shule hivyo vifaa vya ujenzi wa vyumba vya madarasa vitakavyonunuliwa kwa fedha za mapato ya ndani vielekezwe kwenye shule ambazo hazijapata fedha za UVICO-19.

**Azimio**

Mkuu wa Idara ya Elimu awasilishe orodha ya shule zote zilizopata fedha kutoka Srikalini kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

**MUHT.NA.08/FUM/03/29/10/2021/2022: KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022**

Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kuwa, mpango wa manunuzi huandaliwa baada ya mchakato wa bajeti kukamilika wa mwaka husika. Aidha, mpango wa manunuzi unatumika baada ya kuridhiwa na mamlaka husika ambapo kwa upande wa Serikali za mitaa Mamlaka husika ni Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na utawasilishwa kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ndani ya siku 14 baada ya kuridhiwa na mamlaka husika.

Mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha wa 2021/2022 una jumla ya kiasi cha fedha **sh.7,073,283,762.00** kwa mchanganuo ufuatao;

| | | |
|---|---|---|
| i. | Ununuzi wa vifaa | Sh. 2,185,097,136.00 |
| ii. | Ununuzi wa huduma zisizo za kitaalamu | Sh. 364,123,626.00 |
| iii. | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi/miradi | Sh. 4,524,063,000.00 |

Baada ya mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kuwasilishwa wajumbe walipokea, wakaridhia na kushauri taratibu zingine ziendelee.

**MUHT.NA.09/FUM/03/29/10/2021/2022: KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA MAPENDEKEZO YA KUVUNA MAGOGO YA MITI AINA YA MKURUNGU KUTOKA KWENYE MSITU WA HIFADHI WA ULYANKULU.**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, kutokana na azimio la halmashauri la kununua mtambo wa ujenzi wa barabara na kuboresha miundombinu ya barabara kutotekelezwakwa kukosa fedha, inapendekezwa halmashauri ivune magogo katika msitu wa hifadhi wa Ulyankulu yenye mita za

ujazo 3,000. Fedha itakayopatikana itumike kununua greda la kutengenezea barabara. Kiasi cha mita za ujazo 3,000 kitawezesha Halmashauri kupata kiasi cha shilingi 1,050,000,000.00 kwa bei ya chini ya shilingi 350,000.00 kwa mita ya ujazo 1, ambayo ni kwa mijibu wa sheria. Hata hivyo kiasi hicho kinaweza kuongezeka kulingana na makubaliano yatakavyofanyika ya namna ya uuzaji wa magogo hayo. Gharama ya manunuzi ya mitambo ya lutengeneza barabara (Grader, Roller, Excavator, Lori) ni kiasi cha shilingi 1,811,250,000 ($787,500). Taarifa ilieleza kuwa, iwapo kamati itaridhia mapendekezo haya, kusudio hili la Halmashauri litawasilishwa kwenye kamati ya uvunaji endelevu wa mazao ya misitu ya Wilaya kwa hatua zaidi. Baada ya kuwasilishwa wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alipongeza kwa wazo hilo kwani itasaidia barabara nyingi kurekebishwa na kuanza kupitika na kusaidia kutupatia mapato zaidi. Aidha, alishauri kamati zingine ziendelee na utekelezaji wa suala hilo.

Mwenyekiti alipongeza kwa wazo zuri na kushauri kuwa, baada ya mitambo hiyo kununuliwa itumike kama chanzo cha mapato ya Halmashauri. Baada ya mjadala huo wajumbe walipokea na kuridhia wazo hilo na kushauri hatua zingine ziendelee ili kuharakisha suala hilo kukamilika.

**Azimio**

Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili kuhakikisha shughuli za uvunaji wa magogo hayo zinaanza na kusimamia kikamilifu.

**MUHT.NA.10/FUM/03/29/10/2021/2022: KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA MAPENDEKEZO YA MABADILIKO YA BEI ZA VIWANJA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, kutokana na ukuaji wa mji wa Kaliua inayosababishwa na ongezeko la watu sambamba na kuboreka kwa hali ya kiuchumi ya wakazi wa Kaliua pamoja na wawekezaji mbalimbali kuanza kujitokeza wakitaka kuwekeza maeneo mbalimbali ya mji wa Kaliua , mapendekezo ya bei mpya za viwanja yaliwasilishwa kama ifuatavyo;

| S/N | MATUMIZI | BEI/MITA YA MRABA (Tsh) |
|---|---|---|
| 1 | Makazi pekee/Taasisi | 1000/= |
| 2 | Makazi/Biashara | 1200/= |
| 3 | Biashara Pekee | 1400/= |
| 4 | Viwanja | 1500/= |
| 5 | Vituo vya mafuta | 2000/= |

Mwenyekiti alishauri kuendelea kuvitangaza viwanja vinavyouzwa na Halmashauri katika maeneo mbalimbai hasa katika mitandao ya kijamii na kuendelea kutengeneza mazingira mazuri katika viwanja hivyo ili kuweza kuvutia zaidi.

**Hitimisho**

Baada ya ushauri huo wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

**MUHT.NA.11/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MFUKO WA MAENDELEO YA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, Katika kipindi cha roboya kwanza cha Julai – Septemba, 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imeweza kutekeleza zoezi la ufuatiliaji wa marejesho toka kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu vilivyokopeshwa tangu mwaka 2013/2021 na kuweza kufanikisha kurejesha Jumla Sh. 79,799,700.00 kwa mchanganuo ufuatao;

A. Vikundi 47 vya Wanawake vimerejesha Jumlaya Sh. 43,555,200.00
B. Vikundi 19 vya Vijana vimerejesha Jumla ya Sh. 28,397,000.00
C. Vikundi 5 vya Walemavu vimerejesha Jumlaya Sh. 7,847,500.00
**Jumla............... Sh. 79,799,700.00**

**A: FEDHA ILIYOREJESHWA KWA KIPINDI KUANZIA MWAKA 2013 HADI SEPTEMBA, 2021**

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013 hadi Septemba 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imeweza kutekeleza zoezi la ufuatiliaji wa marejesho toka kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu vilivyokopeshwa tangu mwaka 2013/2021 na kuweza kufanikisha kurejesha Jumla **Sh.672,850,050.00** kwa mchanganuo ufuatao.

A. Vikundi vya Wanawake vimerejesha Jumla ya Sh. 431,491,050.00
B. Vikundi vya Vijana vimerejesha Jumla ya Sh. 228,986,000.00
C. Vikundi vya Walemavu vimerejesha Jumla ya Sh. 12,373,000.00
**Jumlakuu Sh. 672,850,050.00**

**B: DENI LILOPO HADI SEPTEMBA, 2021**

Hadi sasa Halmashauri ya Wilaya inaendelea kufuatilia fedha ambayo haijareshwa toka Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu jumla ya **Sh. 1,330,999,950.00** kwa mchanganuo ufuatao

1. Vikundi vya Wanawake bado vinadaiwa jumla ya Sh. 572,758,950.00
2. Vikundi vya Vijana bado vinadaiwa jumla ya Sh. 662,114,000.00
3. Vikundi vya Walemavu bado vinadaiwa Sh. 96,127,000.00

**Jumla Sh. 1,330,999,950.00**

**Changamoto.**

- Vikundi vingi kutozingatia Kanuni na miongozo ya Mikopo
- Idara kutokuwa na gari maalumu kwa ajili ya kufuatilia marejesho

**Mikakati ya kuhakikisha fedha yote iliyokopeshwa inarudishwa**

- Kushirikisha ofisi za kata na vijiji kufuatilia marejesho kwa vikundi vilivyopo katika maeneo yao ya utawala
- Kupeleka mahakamani vikundi sugu
- Idara kufanya ufuatiliaji wa siku kwa siku kwa kila Kikundi kinachodaiwa kwa njia ya kuvitembelea na kuvipigia simu ya kuwahimiza kurejesha.
- Kuvifikisha ofisi za TAKUKURU vikundi ambavyo vinaonesha ugumu na mgomo kabisa wa kurejesha.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alipongeza kwa upangaji wa mikakati ya kuhakikisha marejesho yanakusanywa. Aidha, alieleza kuwa mikakati ya ukusanyaji wa marejesho itakuwa na tija iwapo kutakuwa na ushirikiano katika utekelezaji wa mikakati hiyo.

Mjumbe alishauri kuwa na mawasiliano baina ya Idara ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, Idara ya Fedha na Biashara pamoja na uongozi wa vikundi mbalimbali vilivyokopeshwa vinavyorejesha ili kuwa na taarifa za marejesho zinazofanana.

Mjumbe mwingine alishauri kufuatilia shughuli za msingi wanazofanya katika vikundi wanavyokopeshwa.

Mwenyekiti alieleza kuwa, Idara ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii kuendelea kusimamia mikakati ya kuwafuatilia zaidi vikundi vilivyokopeshwa miaka ya nyuma ili kuweza kufanya marejesho. Aidha, aliwasihi Madiwani kuendelea kuhamasisha urejeshaji wa mikopo hiyo kutoka kwa vikundi walivyokopeshwa.

Ilielezwa kuwa, ushauri uliotolewa umepokelewa na utafanyiwa kazi. Aidha, alishauri viongozi kutumia vikao vya kamati za Maendeleo ya kata kuwa moja ya njia ya uhamasishaji wa marejesho.

**Hitimisho**

Baada ya mjadala huo wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

**MUHT.NA.12/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA TAARIFA YA MAPOKEZI YA GARI LENYE NAMBA ZA USAJILI SU 36793 LILILOKUWA MALI YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA (PSSSF).**

Taarifa ya mapokezi ya gari lenye namba za usajiri SU 36793 kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa UMMA (PSSSF) iliwasilishwa. Taarifa ilieleza kuwa gari hilo lilitolewa kwa

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa barua yenye Kumb. Na. AB.314/431/02/9 ya tarehe 16/09/2021. Hata hivyo hatua hiyo ilifuata baada ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kuwasilisha maombi ya kupatiwa gari kwa Katibu Mkuu – HAZINA kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/CL/80 ya tarehe 28/06/2021 baada ya gari iliyokuwa inatumiwa na Mkurugenzi Mtendaji kutoweza kuhimili shughuli nyingi za Mkurugenzi hivyo, kusababisha matengenezo ya mara kwa mara.

**Hitimisho**

Baada ya taarifa kuwasilishwa, wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

**MUHT.NA.13/FUM/03/29/10/2021/2022:MAOMBI YA IDHINI YA KUTUMIA FEDHA SH. 23,400,000/= KWA AJILI YA MATENGENEZO YA GARI LENYE NAMBA ZA USAJIRI SU 36793**

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala aliwasilisha taarifa ya matengenezo ya gari lenye namba za usajili SU 36793 ambalo limekabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Mkurugenzi Mtendaji alielekeza wataalamu kwenda Arusha kufanya Tathmini ya hali ya gari hilo. Baada ya tathimini kufanyika, ilibainika kuwa gari linahitaji matengenezo kwa kuwa halikuwa likitumika kwa muda. Tathmini ya matengenezo iliyofanywa na fundi ilionesha kuwa zinahitajika **sh. 23,400,000** kwa ajili ya gharama ya kununua vifaa na gharama ya fundi ili gari likamilike na kuweza kutumika.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alishauri kuendelea na utaratibu wa kuomba magari kwa viongozi wa juu kwa kutumia maandiko kwani uwezekano wa kupata magari upo.

Mwenyekiti alipongeza kwa maandiko mazuri ambayo yanaleta tija kwa Halmashauri ya Kaliua hivyo kamati iliridhia matumizi ya fedha kiasi cha sh. 23,400,000/=. Aidha, alishauri fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari ya Mkurugenzi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 zinaweza kutumika kununua magari katika idara mbalimbali.

Baada ya pongezi hizo wajumbe walipokea na kuridhia matimizi ya fedha kiasi cha sh. 23,400,000/= kwa ajili ya matengenezo ya gari yenye namba za usajiri SU 36793.

**MUHT.NA.14/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA MAKISIO YA UJENZI WA KITUO CHA AFYA IGAGALA KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA NJE, MAABARA NA KICHOMEA TAKA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, kutokana na halmashauri kupokea fedha kiasi cha sh. 250,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Igagala. Makisio kwa mujibu wa (Schedule of Materials) na michoro iliyoandaliwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI kama ifuatavyo;

| | |
|---|---|
| Jengo la OPD | sh. 170,446,255.23 |
| Jengo la Maabara | sh. 93,275,195.05 |
| Kichomea taka | sh. 7,313,760.00 |
| **Jumla** | **SH. 271,035,210.73** |

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea na kushauri utekelezaji wa shughuli katika utekelezaji wa mradi huo uendelee.

Azimio

Utekelezaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya Igagala uanze mapema.

**MUHT.NA.15/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPITIA NA KUIDHINISHA TAARIFA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA NA VITENGO KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA, 2021**

**15.1. Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji**

Taarifa iliwasilishwa na Mkuu wa Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji ikionesha utangulizi, kazi zilizopangwa kutekelezwa mwezi Julai hadi Septemba 2021 ambazo ni pamoja na Uandaji na uwasilishaji wa taarifa ya Laac 2019/2020 ambapo Taarifa iliandaliwa na kuwasilishwa katika Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Ufuatiliaji wa miradi ya elimu itakayopatiwa vifaa vya ujenzi ambapo ufuatiliaji wa miradi ya elimu ya msingi na sekondari itakayopatiwa vifaa vya ujenzi umefanyika, Uandaaji wa Mpango Mkakati wa halmashauri 2021/2022-2025/2026 ambapo Maandalizi ya Mpango Mkakati wa Halmashauri yanaendelea na rasimu imewasilishwa katika kamati ya Fedha ,Uongozi na Mipango, uandaaji wa taarifa ya miradi kwa robo ya I kwa mfumo wa MEF na CDR ambapo uandaaji wa taarifa unaendelea na zikikamilika zinawasilishwa ofisi ya katibu Tawala (M)

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuiridhia.

Mwenyekiti alieleza kuwa,kwa shule za Msingi, shule za kimkakati zipatiwe kipaumbele na sekondari kuzipa kipaumbele kata ambazo hazina shule za sekondari. Aidha, aliongeza kuwa, Idara ya Mipango na Ufuatiliaji inatakiwa kuzingatia maoni ya wananchi kabla ya kuanzisha miradi katika ngazi za chini. Baada ya maoni ya Mwenyekiti wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

## 15.2. Idara ya Utumishi na Utawala

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala aliwasilisha taarifa ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021 ikiwa ni pamoja na Kuandaa na Vikao vitatu vya Menejimenti vimefanyika tarehe 05/07/202106/08/2021 na tarehe 07/09/2021. Aidha, Vikao vitatu vya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango vimefanyika tarehe 16/08/2021, 17/08/2021 na tarehe 18/08/2021. Vikao vya Kamati za Kudumu vya robo ya pili vilifanyika kama ifuatavyo:

- Kamati ya Elimu, Afya, na Maji tarehe 10/08/2021
- Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira tarehe 09/08/2021
- Mkutano wa Baraza la Madiwani tarehe 30-31/01/2021
- Kamati ya Kudhibiti UKIMWI12/08/2021

Kuandaa na kuratibu ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ambapo wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango walifanya Ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo tarehe 16/08/2021 hadi tarehe 18/08/2021, Kuhakikisha malipo ya mishahara ya Watumishi wote wa Halmashauri yameandaliwa na kulipwa katika kipindi chote cha miezi mitatu cha Januari hadi Machi 2021 ambapo idara imeandaa mishahara ya miezi mitatu ya Watumishi 2434 wa halmashauri yenye thamani ya Ths. 5,032,795,950/= kwa mchanganuo ufuatao

- Mwezi Julai tsh. 1,670,953,650.00
- Augusti tsh. 1,684,245,150.00
- Septemba tsh.1,677,597,150.00

Kushughulikia malipo ya wastaafu na mafao mengine ya watumishi ambapo fomu za mafao za wastaafu wawili (02) kutoka Idara ya elimu msingi na Idara ya Fedha na biashara

- Gration Kashoro Gerase
- Muzanye Costa Thadeo

Aidha mafao ya uzazi ya watumishi tisa na moja (09) yaliandaliwa na kuwasilishwa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF). Watumishi hao ni:

- Rhoida William Sokoni
- Siwema John Wandela
- Lusia Kileo Joseph
- Eva Mshiko James
- Devotha Peter Msea

- Mboka Enock Mwakapala
- Faraja Omari Mswima
- Grace Emily Kessy
- Mhindi Mganga Joseph

Kufanya ufuatiliaji wa vikao na mikutano ngazi za kata na vijiji na kukagua utekelezaji wa shughuli za serikali pamoja na kuhakikisha vikao/mikutano yote ya kisheria inafanyika kwenye kata 25 na vijiji 88 ambapo Idara imeendelea kuwakumbusha watendaji wa kata na vijiji kufanya Mikutano mikuu kwa kuzingatia ratiba ya vikao hivyo na kusisitiza kuweka Agenda za kudumu zikiwemo kusoma taarifa za mapato na matumizi ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji, taarifa za ulinzi na usalama kusimamia shughuli za maendeleo na kujadili masuala ya jinsia na Ukimwi.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alishauri Mkuu wa Idara ya Utumishi na utawala kufuatilia suala la Watendaji wa kata na Vijiji kutokuwepo kwenye maeneo yao ya kazi wakati wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wanapofika kutembelea miradi.

Mjumbe alishauri kupata mtendaji atakayekwenda katika kijiji cha Ntwigu kwani hakuna mtendaji kwa muda mrefu na kusababisha shughuli za maendeleo kusimama.

**Muuguzi wa zahanati ya Kashishi kuondolewa**

Mjumbe alieleza kuwa, kuna muuguzi wa zahanati ya Kashishi amekuwa akisababisha vifo vya watoto wanaozaliwa na kuwasumbua wanawake wanafika kujifungua na hali hii imesababisha wananchi kutokuwa na imani na mtumishi huyo hivyo alishauri aondolewe ili isitokee vurugu.

Mwenyekiti alieleza kuwa, Kashishi kuna changamoto kubwa kwani mtumishi huyo amekuwa akisumbua wananchi na kushindwa kutoa huduma kwa wakati. Aidha, aliongeza kuwa, Kashishi panatakiwa kufanyiwa kazi kutokana na tabia ya mtumishi huyo. Pia alishauri kuendelea kushughulikia tabia za watumishi wanaoonekana kutokuwa na nidhamu.

**Ushirikiano baina ya viongozi wanaopatikana ngazi ya Kata**

Mwenyekiti alieleza kuwa, katika maeneo mengi yaliyotembelewa na wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwenye ziara ya wajumbe wa kamati ya fedha iliyofanyika tarehe 20-24/10/2021 wananchi na viongozi wengine hawashiriki kwenye ziara pia baadhi ya watendaji wamekuwa hawafiki kwenye eneo la mradi. Aidha, alitoa mfano mtendaji wa Igombe, Usenye na maeneo mengine.

Ilielezwa kuwa, yaliyozungumzwa na kushauriwa yamechukuliwa na yataendelea kufanyiwa kazi. Baada ya mjadala na maelezo hayo wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

### 15.3. Idara ya Fedha na Biashara

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021 ambazo ni pamoja na Kukusanya Maduhuli ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na;

- Kusimamia ukusanyaji wa ushuru wa mazao magetini
- Kusimamia ukusanyaji wa ushuru wa minadani

Ambapo Ukusanyaji wa Ushuru wa mazao mbalimbali kutoka mageti 23 ya kukusanyia ushuru wa mazao ambayo ni Kashishi, Ulyankulu, Ibambo, Mwamnange, Mpandamlowoka, Usinge, Kamsekwa, Usindi, Usimba, Ugunga, Seleli, Zugimlole, Nhwande, Usinga, Isawima, Makubi, Ulanga, Mwaharaja, Kaliua Mjini, Konamoja, Konanne, Igombe na Malanga. Aidha, Katika vyanzo vya mazao, kiasi cha shilingi 1,077,417,675.00 zimekusanywa kwa miezi mitatu sawa na 381.39% ya lengo la robo ya kwanza la kukusanya 282,500,000.00, kusimamia ukusanyaji wa ushuru wa minada ambapo halmashauri ya Wilaya ya Kaliua inayo minada 9 ya mifugo. Katika miezi mitatu, Julai hadi Septemba 2021, Idara imesimamia ukusanyaji katika chanzo hiki na jumla ya shilingi 117,442,015.00 sawa na 128.93% ya lengo la robo ya kwanza la kukusanya 91,091,000.00, Kusimamia utoaji wa Leseni za Biashara ambapo jumla ya leseni 349 za biashara mbalimbali zimetolewa Julai hadi Septemba, 2021. Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alieleza kuwa, Usenye panatakiwa kuwa na mashine ya kukusanyia mapato (POS) kutokana na kuwa na mazao mengi pamoja na magari mengi yanayofika kuchukua mazao mbalimbali katika Kata hiyo.

Mwenyekiti alieleza kuwa, idara ya fedha ifanyie kazi suala la kupeleka mashine ya kukusanyia mapato (POS) katika kata ya Usenye ili kuendelea kukusanya mapato. Aidha, alishauri kuendelea kuibua vyanzo vipya vya mapato. Aidha, alishauri itengenezwe sehemu ya maegesho ya magari katika eneo la ISAWIMA ambapo magari yanayoegeshwa pembeni mwa barabara ni mengi na kushindwa kufika kuegesha magari Kaliua. Baada ya maelezo hayo wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

### 15.4. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani aliwasilisha taarifa ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021 ambazo ni pamoja na Ukaguzi wa taarifa za Kifedha na kuhakikisha Halmashauri inatekeleza mapendekezo ya Mkaguzi wa Nje (CAG) na mapendekezo ya Mkaguzi wa Ndani umefanyka, mkaguzi mifumo ya udhibiti wa ndani(Internal Control) katika Idara zote za Halmashauri umefanyika, ukaguzi wa mikataba na taratibu

za manunuzi umefanyika, Ukaguzi wa mishahara na Madai ya watumishi, kupitia na kukagua taratibu za ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mfumo LGRCIS kama zinafuata taratibu na mapato yanawasilishwa benki kwa mujibu wa Menmoranda ya fedha za Serikali za Mitaa kwa umefanyika.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo;

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alishauri Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kuendelea kufanya ukaguzi katika ngazi za chini ili kuondokana na changamoto zinazoweza kujitokeza kwenye ukaguzi kwani hoja nyingi zinazopatikana hutokea katika miradi ya ngazi za chini.

Mjumbe alishauri Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kufanya uthamini wa majengo ya Halmashauri kama vile jengo la Ofisi ya Mkurugenzi.

Ilielezwa kuwa, uthamini wa majengo hufanyika kila baada ya miaka mitano (5) na haufanywi na halmashauri.

Mwenyekiti alipongeza kitengo hicho kwa kazi nzuri inayoendelea kutekelezwa na Kitengo hicho. Aidha, alishauri kufuatilia maeneo ambayo wamepewa saruji nyingi na maeneo ambayo miradi imesitishwa ili mapungufuya kiutendaji yasijitokeze.

Baada ya mjadala huo wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

**15.5. Kitengo cha TEHAMA.**

Kaimu msimamizi wa kitengo cha TEHAMA aliwasilisha taarifa ya shughuli mbalimbali zilizotekel ezwa katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021 na utekelezaji wake Kusimamia ukusanyaji wa mapato magetini, POS Mashines zimekaguliwa, Kutoa mafunzo kwa watumiaji wa vifaa vya TEHAMA kwa asilimia zaidi ya 75, Mafunzo kwa watumiaji wa POS mashine yamefanyika, Msaada wa kitaalam kwa watumiaji wa vifaa vya TEHAMA umetolewa kwa zaidi ya asilimia 75, Usimamizi wa mifumo na utoaji wa ushauri wa kitaalam kwa watumiaji wa vifaa vya TEHAMA yametolewa kwa zaidi ya asilimia 75, CCTV camera zinafanya kazi vizuri, kuweka ant-birus katika kompyuta zote za Mkurugenzi Mtendaji ambapo Anti-virus zimewekwa katika kompyuta zote za Mkurugenzi Mtendaji, kuchukua matukio yote na kurusha kwenye mitandao ya kijamii ambapo matukio yamechukuliwa na kurushwa kwenye mitandao ya kijamii pamoja na tovuti ya Halmashauri kwa asilimia zaidi ya 75.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuridhia taarifa hiyo.

### 15.6. Kitengo cha Manunuzi na Ugavi

Kaimu Mkuu wa kitengo cha manunuzi na Ugavi aliwasilisha taarifa ya shughuli mbalimbali zilizot ekelezwa katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021 na utekelezaji wake ambazo ni pamoja na kuendelea na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara, kichomea taka, duka la dawa, wodi ya wanaume,wodi ya wanawake pamoja na wodi ya watoto, Kuendelea na Matengenezo ya magari na service za magari ambapo **matengenezo ya magari ambapo imetengenezwa gari** ambulance Land Cruiser DFPA, gari Nissan DFPA, gari Land Cruiser STK Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi na ukamilishaji wa miradi ya madarasa shuleni, Ununuzi wa saruji 1294 kwaajili ya ujenzi ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (Utengenezaji wa kebston na kumwaga zege), Ununuzi wa BRC na Marine bodi kwaajili ya ujenzi wa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Ununuzi wa saruji 997 kwaajili ya ujenzi wa shule ya mchepuo wa Kiingereza, Ununuzi wa vifaa vya ujenzi na usafi shule ya Mchepuo wa Kiingereza.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alishauri vifaa vya ujenzi viwe vinanunuliwa mapema ili kusaidia usafirishaji usiwe mgumu kwa maeneo yasiyopitika wakati wa masika. Aidha, alishauri vifaa vya ujenzi vya upande wa Ulyankulu visogezwe Ulyankulu visipokelewe Kaliua na kufuatwa na wahusika.

Mjumbe mwingine aliomba kusaidia kupata mabati katika mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari ya Mpandamlowoka.

Mwenyekiti alishauri taratibu za manunuzi zifuatwe. Aliongeza kuwa, kufanya ufuatiliaji kwa maeneo wanayopelekewa vifaa na kununua vifaa vya ujenzi kwa kuzingatia mahitaji.

Ilielezwa kuwa, taratibu za manunuzi ya saruji mifuko 2400 zinaendelea na wazabuni wanaotakiwa kuleta saruji wanaendelea kufuatiliwa. Baada ya maelezo hayo wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

### 15.7. Kitengo cha Sheria

Kaimu Mkuu wa kitengo cha sheria aliwasilisha taarifa ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021 ambazo ni pamoja na Kutoa elimu kwa wajumbe wa mabaraza ya kata juu ya uendeshaji wa mabaraza ambapo mafunzo ysmetolewa kwa mabaraza ya kata ya Kaliua, Igagala na Usinge, Kufanya upekuzi wa mikataba baina ya Halmashauri na wadau wengine, mikataba ya ujenzi wa josho katika mnada wa Ugansa imeweza kukaguliwa kabla ya kusainiwa pamoja na Kutoa ushauri wa kisheria, kazi zitakazo tekelezawa katika kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba, 2021 pamoja na ikama ya kitengo cha sheria. Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kujadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alitaka kufahamu sifa/vigezo vya waombaji wa wajumbe wa mabaraza ya Kata hasa katika suala la umri.

Ilielezwa kuwa, kuhusu kigezo cha umri ni kuanzia miaka 18 na kuendelea na haina kikomo cha msingi isiwe umri ambao mjumbe anaweza akashindwa kutekeleza majukumu yake.

Sheria ndogo za madini

Mwenyekiti alitaka kujua kuhusu hatua iliyofikiwa katika ushughulikiaji wa suala la sheria ndogo za madini. Aidha, alitaka kujua pia hatua iliyofikiwa katika kesi ya halmashauri kuhusu magogo.

Ilielezwa kuwa, suala la sheria ndogo za madini linaendelea kushughulikiwa na taarifa itawasilishwa kwenye Baraza la Madiwani ili kupata kibali cha kuendelea na utaratibu. Aidha, aliongeza kuwa, kesi ya magogo ipo polisi na polisi nab ado haijapelekwa mahakamani kutokana na kuendelea na uchunguzi.

**15.8. Kitengo cha Uchaguzi**

Mkuu wa kitengo cha Uchaguzi aliwasilisha taarifa ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021 ambazo ni pamoja na kuhamisha vifaa na nyaraka za uchaguzi Mkuu zilizobaki katika ukumbi mdogo wa halmashauri baada ya zoezi la uteketezaji kuvipeleka shule ya sekondari kaliua kwa ajili ya kuhifadhiwa kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambapo zoezi la kuhamisha vifaa vifaa na nyaraka kutoka ukumbi mdogo wa halmashauri lilifanyika kuanzia tarehe 12/07/2021 hadi 14/07/2021 ambapo masanduku na vitutuli vilihamishiwa katika ghala lililopo shule ya sekondari Kaliua. Taa na nyaraka zilizobaki baada ya zoezi la uteketezaji kwa maelekezo ya Tume vilihamishiwa katika ghala dogo la Halmashauri, kuratibu vikao viwili vya Kamati ya Ukaguzi kwa robo ya kwanza kipindi cha Julai hadi Septemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo jumla ya vikao viwili vya Kamati ya Ukaguzi viliratibiwa ambapo kikao kimoja kilifanyika tarehe 24.09.2021 kikiwa ni kikao maalum kwa ajili ya kupokea, kuipitia, kujadili na kutoa ushauri kuhusu Kitabu cha Hesabu za Halmashauri za mwaka 2020/2021. Aidha, kikao kingine kilifanyika tarehe 29.09.2021 kwa ajili ya kujadilili na kutoa maoni kuhusu taarifa mbalimbali na hoja za Mkaguzi wa ndani kwa robo ya nne ya mwaka 2020/2021.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa hiyo.

Baada ya taarifa zote kuwasilishwa wajumbe walipongeza Idara zote zilizowasilisha taarifa za utekelezaji na kushauri kuendelea kuwa na ushirikiano ili kuweza kutekeleza mipango mikakati inayopangwa.

**MUHT.NA.16/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA ZABUNI MBALIMBALI ZILIZOPITISHWA NA BODI YA ZABUNI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, kutokana na taratibu za kupata wazabuni wanaotakiwa kufanya kazi na Halmashauri inatakiwa kuwa na wazabuni waliopitishwa kisheria kufanya kazi na Halmashauri, tunawasilisha wazabuni waliopitishwa na Bodi ya zabuni kwa ajili ya kufanya kazi

na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.Baada ya taarifa kuwasilishwa, wajumbe walipokea, wakaridhia na kushauri utaratibu uendelee ili shughuli zianze kutekelezwa.

**MUHT.NA.17/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA, KUPITIA NA KUJADILI MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI KUHUSU TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA KWANZA JULAI – SEPTEMBA 2021 (2021/2022)**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha taarifa ya marejesho ya mikopo ya makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kipindi cha robo ya kwanza 2021/2022, taarifa ya mkaguzi wa Ndani robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo Mkaguzi wa ndani aliwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa hoja za ukaguzi katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 kuwa ni asilimia sitini na nne desimali mbili (64.2%) ya hoja za ukaguzi zilizoibuliwa katika kipindi cha robo ya kwanza. Hoja zote 14 zilizoibuliwa zilitokana na udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha na matumizi ya vifaa na huduma. Jedwali linaonesha kiwango cha utekelezaji wa hoja hizo;

| Na | MAELEZO | IDADI YA HOJA ZILIZOIBULIWA | ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|
| 1 | Hoja za robo ya kwanza | 14 | 100% |
| 2 | Idadi ya Hoja zilizotekelezwa | 9 | 64.2% |
| 3 | Hoja zinazoendelea kutekelezwa | 5 | 35.8% |
| 4 | Idadi ya hoja ambazo hazijatekelezwa | 0 | 0% |

**Hitimisho**

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea, wakaridhia kukubaliana kuwa, wanaohusika kujibu hoja zilizoibuliwa wafuatiliwe na kutoa majawabu ya hoja hizo na viambata vyake. Aidha, wajumbe walikubaliana na maoni ya Mkaguzi katika hoja hizo.

**MUHT.NA.18/FUM/03/29/10/2021/2022:TAARIFA ZA SERIKALI**

*i. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha* ***Sh. 3,700,000,000.00*** *na Ombi la Idhini ya Kufanya Uhamisho wa Fedha Nje ya Bajeti (****Reallocation Between****) ya Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19*

Taarifa iliwasilishwa kuwa, tarehe 19/10/2021 Halmashauri ya wilaya ya Kaliua ilipokea fedha sh. 3,700,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Fedha zilizopokelewa ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 86 vya madarasa katika shule za Sekondari 20 na ujenzi wa vyumba 99 vya madarasa shule shikizi 20. Fedha hizi zimeingizwa moja kwa moja katika akaunti za shule husika na ujenzi wa miradi husika unatakiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021. Aidha, kwa kuwa fedha hizi hazikuwa kwenye Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022, Menejimenti inaomba idhini ya kufanya uhamisho wa nje wa bajeti (Reallocation Between) ili fedha hizi ziweze kutumika kutekeleza shughuli zilizokusudiwa.

Baada ya taarifa kuwasilishwa, wajumbe walipokea, wakaridhia na kupongeza serikali kwa kuleta fedha hizo na kushauri kusimamia matumizi ya fedha hizo kwa ushirikiano. Aidha Mwenyekiti alishauri orodha ya shule zilizopata fedha hiyo zibandikwe kwenye ofisi mbalimbali ili kuweka uwazi kwa wananchi na kushauri utekelezaji uendelee.

*ii. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha **Sh. 368,117,139.58** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo*

Taarifa iliwasilishwa kuwa, mwezi Oktoba 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilipokea fedha Sh. 368,117,139.58 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha hizi zimegawanyika katika mchanganuo ufuatao;

a) Mradi wa WASH 2020/2021........................Sh. 232,500,000.00

b) Fedha za EP4R.......................................Sh. 135,617,139.58

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe walipokea, wakaridhia na kushauri utekelezaji uweze kuendelea.

*iii. Taarifa ya vijiji vilivyoruhusiwa kuendelea kuwa vijiji halali vilivyokuwa kwenye Hifadhi za Misitu ya Ulyankulu, Igombe, Mpandaline na North Ugala*

Taarifa iliwasilishwa ikionesha vijiji vilivyoruhusiwa kuendelea kuwa vijiji halali vilivyokuwa kwenye Hifadhi za Msitu wa Ulyankulu, Igombe, Mpandaline na North Ugala. Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo;

Mwenyekiti alitaka kujua iwapo uchambuzi huo umezingatia vijiji vilivyozaliwa kutoka kwenye vijiji vingine. Aidha, alitaka kufahamu vijiji ambavyo havijatajwa na kata zao.

Ilielezwa kuwa, kilichozingatiwa ni mwongozo. Vijiji ambavyo havijatajwa vitahakikiwa na wataalam kutoka Wizarani kulingana na mwongozo. Aidha, alieleza kuwa, vijiji vilivyoruhusiwa vimepewa maelekezo.

Mwenyekiti alieleza kuwa, taarifa hiyo haijakamilika kutokana na kutokuwa na baadhi ya taarifa muhimu.

Katibu alieleza kuwa, suala hilo linachukuliwa na Idara ya Ardhi na Maliasili kwenda kuiandaa taarifa hiyo kikamilifu

*iv. Taarifa ya mapokezi ya Fedha sh. 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ilege*

Taarifa iliwasilishwa kuwa, Tarehe 21/10/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilipokea fedha kiasi cha sh. 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Ilege. Mradi huu unatekelezwa kutokana na mapato ya Serikali yanayopatikana kutoka kwenye tozo za miamala ya simu, ili kuboresha huduma za kijamii za afya, Elimu, maji na barabara. Aidha, majengo yaliyokusudiwa kwa ajili ya ujenzi huo ni pamoja na jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la maabara na kichomea taka na ujenzi huu utafanyika kwa njia ya Force Account, kwa mujibu wa Mwongozo wa ujenzi kwa kutumia Kikosi Kazi (Force Account) uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) mwezi Mei 2020. Baada ya kuwasilishwa wajumbe walipokea na kupongeza Serikari kwa kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kiasi hicho cha fedha kwa ajili mradi huo.

**MUHT.NA.19/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA OMBI LA SHULE YA SEKONDARI YA ULYANKULU KUNUNUA VIFAA VILIVYOPO KATIKA ZAHANATI YA MAKONGE**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, shule ya sekondari ya Ulyankulu imepokea sh. 200,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa kwa kuwa zahanati ya Makonge ina saruji mifuko 1050 na kwa kuwa uendeshaji wa shughuli za ujenzi katika zahanati hiyo umesitishwa, inaombwa idhini ya shule ya sekondari Ulyankulu kununua Saruji na Vifaa vingine vilivyopo katika zahanati hiyo ili;

i. Kuharakisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari Ulyankulu

ii. Ili kuokoa vifaa vilivyopo katika zahanati ya Makonge visiharibike

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walipokea na kuridhia ombi hilo. Aidha, walishauri utekelezaji uendelee. Pia mwenyekiti alishauri kuwashirikisha viongozi wa eneo la makazi na Afisa Tarafa kwa hilo.

**MUHT.NA.20/FUM/03/29/10/2021/2022:KUPOKEA NA KURIDHIA TAARIFA YA MATUMIZI YA VIFAA VYA UJENZI WA KITUO CHA AFYA UYOWA KUTUMIKA.**

Taarifa iliwasilishwa kuwa kutokana na kusitishwa kwa shughuli za ujenzi wa kituo cha Afya cha Uyowa baadhi ya vifaa vya ujenzi vinaweza kuharibika. Hivyo iliombwa idhini ya kuvitumia vifaa ambayo vinaweza kuharibika iwapo vitaendelea kuhifadhiwa ili viweze kutumika katika ujenzi wa majengo hayo.

Baada ya kuwasilishwa wajumbe walipokea na kuridhia ombi la kutumia vifaa hivyo.

**MUHT.NA.21/ FUM/03/29/10/2021/2022: TAARIFA YA ZIARA YA WAJUMBE WA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO YA TAREHE 20-24/10/2021**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, ilifanyika ziara ya wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kuanzia tarehe 20-24/10/2021 ambapo wajumbe walitembelea katika miradi mbalimbali kama ifuatavyo; Mradi wa zahanati ya Luganjo mtoni, ujenzi wa kituo cha Afya Usinge, ujenzi wa uzio wa mnada wa Ugansa, ujenzi wa miundombinu katika shule shikizi ya Muungano, ujenzi wa kituo cha Afya Igagala, ujenzi wa shule ya mchepuo wa kiingereza, ujenzi wa jengo la utawala shule ya sekondari ya Ukumbisiganga, ujenzi wa zahanati kijiji cha Igombe, ujenzi wa miundombinu shule shikizi ya Ibumba, ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya msingi Mnange, ujenzi wa kituo cha Afya Uyowa, upanuzi wa zahanati ya makonge, ujenzi wa zahanati kijiji cha Usonga, ujenzi wa zahanati kijiji cha Utantamke, ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya msingi Kadutu na ujenzi wa kituo cha Afya Mwongozo. Aidha katika Majumuisho ya ziara ya wajumbe wa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wajumbe walijadili kama ifuatavyo;

Mjumbe alishauri, Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kuendelea kukagua maeneo mbaimbali yenye miradi katika ngazi za chini inayotekelezwa na fedha za wananchi na nyinginezo.

Mjumbe mwingine alishauri, wataalam na wananchi kuwa na ushirikiano katika utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyoanzishwa katika sehemumbalimbali za Halmashauri ya Kaliua.

Mjumbe alishauri, watumishi kuendelea kuheshimu viongozi na kuhakikisha wanakuwepo kwenye maeneo ya mradi wakati wa ukaguzi wa mradi.

Mwenyekiti alishauri ujenzi wa shule yamchepuo wa kiingereza ufanyike kawaida na siyo ghorofa iwapo itahitajika kufanya hivyo ni kwa baadaye wakati wanafunzi wanaendelea kusoma. Aidha alisisitiza watumishi kuheshimu viongozi wao ili kuweza kuleta maendeleo katika halmashauri ya Kaliua.

Baada ya mjadala huo wajumbe kwa pamoja walikubaliana na kuazimio kama ifuatavyo;

**Azimio**

**MUHT.NA.22/ FUM/03/29/10/2021/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hapakuwa na mengineyo katika kikao hicho

**MUHT.NA.23/ FUM/03/29/10/2021/2022: KUFUNGA KIKAO**

Katibu kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki vyema kwenye kikao na kushukuru kwa kutoa idhini ya vitu mbalimbali. Baada ya kueleza hayo alimkaribisha mwenyekiti ili aweze kufunga kikao. Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti alieleza kuwa, kulikuwa na suala la kuwa na Chuo Kikuu katika Mkoa wa Tabora na ilishauriwa kuwa suala hilo linatakiwa kujadiliwa kwa wananchi, baada ya wananchi kuafiki lijadiliwe kwenye vikao vya Timu ya wataalam wa halmashauri (CMT), Kamati na Baraza na hatimaye kufika katika ngazi za juu. Pia alishauri kuwa na usiri wa vikao na kuwa na ushirikiano. Baada ya kusema hayo, alifunga kikao saa 12:00 jioni.

**UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA:**

| | |
|---|---|
| **SAINI**............................... | **SAINI**............................... |
| **Jina**....Jerry D. Mungo.... | **Jina**....Jahael M Lufungija.... |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| **TAREHE**....19/11/2021.... | **TAREHE**....19/11/2021.... |